

FD

a mamlaka  
nalenga ka-  
na matatizo  
mnapaswa  
matatizo ya  
ni wale wa  
ngi wao ni  
resha utoaji  
vananchi na  
ijenzi wa vy-  
isa, nyumba  
vyaa afya na  
na salama.  
nzi wa Mam-  
Mitaa, Nuru  
na katika ki-  
ada 21 zime-  
o zimelenga  
funza mam-  
o ni msingi  
majukumu



(kushoto,  
kwa'  
iphace  
a TUICO

eleo

va Ujenzi  
f. Makame  
mba Cha-  
kushiriki-  
lli kuwatu-  
uzania.  
Chamuritho  
d makini  
na ambaye  
makuhwa  
katika ku-  
zama wa-  
simu iliyio  
Makame.

## Sheria, kanuni sekta ya uvuvi kuboreshwa

Na Paul Mabeja, DODOMA

SERIKALI inafanya mapitio ya sheria na  
kanuni zinazosimamila sekta ya uvuvi ili  
kukuza na kuendeleza viumbe maji.

Moja ya njia za kukuza na kuendeleza  
viumbe halilili pamoja na ufugaji samaki  
kwa kutumia vizimba.

Wazirii wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba  
Ndaki, alibainisha hayo jijini hapa alipo-  
zungumza na waandishi wa habari baada  
ya kushiriki mkutano wa kimatalifa wa  
kukuza na kuendeleza ukuzaji viumbe  
maji ulifanyika kwa njia ya mtando.

Mashimba, alisema lengo la kupitia she-  
ria pamoja na kanuni katika sekta hiyo ni  
kuhakikisha kuwa zinawezesha uvuvi wa  
kutumia vizimba pamoja na mabwawa.

"Sheria pamoja na kanuni zetu awali  
sektu hili ya uvuvi ilikuwa imemezwa na  
uvuvi wa majini tuu hivyo tunafanya  
mapitio ili kuwezesha uvuvi huu wa  
kutumia vizimba unakuwa na mchango  
katika kuongeza pato la taifa," alisema  
Mashimba.

Akizungumzia mkutano huo, alisema  
lengo lake ni kuwezesha nchi washiriki  
kukuza na kuendeleza ukuzaji wa viumbe  
maji kwa kutumia uvuvi wa vizimba, ma-  
bwawa pamoja na njia nydingene zisikwa  
za bahari au ziwa.

"Pia katika mkutano huu tunaangalia  
changamoto pamoja na fursa zilizopo,  
vipaumbele na namna ya kuendeleza  
uvuvi wa viumbe maji," alisema.

Alisema uvuvi huo una mchango mkub-  
wa katika usalama wa chakula ambapo  
hivi sasa sekta hiyo inachangia pato la  
taifa kwa asilimia 1.7.

"Kwenye samaki tunapata protini kwa  
asilimia 21 na takwimu zinaonyesha kuwa  
kuna kipindi tulipanda hadi kuflikia mtu  
mmoja kula kilo 14, kwa mwaka lakini  
mwaka 2020, tumeshuka hadi mtu mmoja  
kula kilo 8.5 kwa mwaka," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema Taifa  
linatakiwa kuwa na uvuvi endelevu un-  
aochangia usalama wa chakula na kuka-  
biliana na mabadiliko tabianchi.

"Tumekubiliana kuwa na ushirikiano  
wetu wa namna ya kuceana utaalamu wa  
kukabiliana na mabadiliko tabianchi ili  
kuwa na uvuvi endelevu utakaokuza pato  
letu lakini pia pato la dunia kupitia sekta  
hili," alisiasitiza.

Vilevile, alisema mkakati wa serikali ni  
kuhakikisha inafanya utafiti wa maeneo  
kwa ajili ya ufugaji samaki kwa njia ya  
vizimba.

"Ili kuwasaidia watu wanaohitaji kufuga  
samaki kwa njia hili serikali inafanya  
utafiti wa mazingira kwa ajili ya ufugaji  
ili kuwaondolea gharama wananchi  
watakahitaji kwa kuwa gharama zake ni  
kubwa," alisema.

Kadhalika, alisema mkakati mwininge  
ni kuhakikisha kuwa vituo vitano vya  
ukuzaji viumbe maji vinaboresha na ku-  
zalisha vifaranga vya samaki kwa wingi  
na vyenyé ubora.

"Lakini serikali inampingo wa kuanzi-  
sha mashamba darasa kila wilaya kwa  
ajili ya kufundisha wakulima pamoja na  
wafugaji ufugaji wa samaki kwa kutumia  
vizimba na mabwawa," alisema.